KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

15/= Ksh

Volume 28

13th Rabi ul-Awwal 1434

25th Jan, 2013

VIKOMO 12 KWA WENYE KUSHEREHEKEA MAWLIDI YA MTUME

NA: THE QUR'AN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST-AFRICA

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

MILAAD UN-NABI	1 - 4
LUGHA YA KISWAHILI	1 - 4
HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR	

SHENG INANAJISI KISWAHILI

Sheng ama lugha simo ni lugha inayotumiwa na watu wa kundi maalum kwa ajili ya kutaka waelewane wao kwa wao na pengine kuwatenga watu wengine. Katika mukhtadha huo ni sawa kusema kuwa ni lugha isiyokuwa na mfumo wa rasmi wa sarufi kwani watu hubuni majina wanavyofikiria.

Majina yanaweza kubuniwa kutoka kwa vipande vya lugha tofauti, kubadilisha maneo kwa mfano kutoka nyuma ukirudi mwanzo na kadhalika. Kwa mfano neno bata unaweza kuwasikia vijana wakenya wakisema taba na kuoga wanasema kugao.

Nimeanza na maelezo hayo kuonyesha namna lugha hiyo inayotajwa kuwa ya kihuni na baadhi ya wasomi wa Kiswahili inatofautiana kutokana na mtu anachosema na mahali anaposemea.

Hata hivyo kwa wataalamu wa isimu jamii (social linguists) watakupiga mawe ukikashifu matumizi ya sheng. Wengine hata

(Endelea Uk. 4)

Kila sifa njema ni zenye kumthubutukia Mola wa viumbe vyote na Rehema na Amani zimteremkie Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) aliye mbora wa wana-Adamu wote, Amma Ba'd:

Natarajia kuweka mbele ya macho ya msomaji, vikomo vifuatavyo (venye kukukomesha usiendelee na jambo hilo (kama alama za makatazo) kuhusu kusoma mawlidi, kulingana na Uislamu na Shariah zake, jambo lililo halali. Au kinyume na Uislamu! Kwa muelekeo mwengine yaani yastahiki mtu kupata jazaa au adhabu! Na zaidi namuomba Mola, kuwa makala haya yatakuwa ni ya manufaa kwa wote.

KIKOMO CHA KWANZA:

Allaah (تبارك وتعالى) alimuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kufuata kile alichokiteremsha kwake na wala asizue, na ingawa amesema katika Qur'aan: **"Kisha tukakuweka wewe juu ya Njia ya haya mambo, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wasio jua kitu."** [ALJATHIYA 45:18]

Matendo ya ibada ya Kiislamu hayabadiliki, hayashikwi na ugonjwa na ni ya daima kama yalivyoteremshiwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hamna nafasi ya bongo kuyaingilia hayo. Kwahivyo Allaah alimuarisha Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) kuyafuata yaliyoteremshwa kwake katika misimamo mingi. Kwa mfano maneno ya Allaah katika Qur'an: **"Na usipowaletea Ishara waitakayo husema: Kwa nini hukuibuni? Sema: mimi ninafuata yanayofunuliwa kwangu kutokana na Mola Mlezi wangu. Hii (Qur'ani) ni hoja zinazotoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema kwa watu wanaoamini."** [AL-A'ARAAF 7: 203).

Na zaidi, wanavyuoni wa Ki-Islamu wa kikweli wamesuluhisha kuwa kufanya ibada ni kwa kufaulu kwa Qur'aan na Sunnah na sio kuzua wala kubuni jambo.

KIKOMO CHA PILI: Kwa hakika Allaah (سبحانه وتعالى) Aliwapa waumini ne'ma kubwa kwa kuwatumia Mtume Wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم) wala sio *BIRTHDAY* yake kabisa. Hilo ndilo Alisemalo Allaah (سبحانه وتعالى) katika kitabu Chake Al-Qur'aan: **"Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu (Qur'aan) na hikima (Sunnah), ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi."** [Aal-I'mraan 3:164].

KIKOMO CHA TATU: As-Salaf wa kwanza wa Kiislamu ambao waliokuwa ni Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) (*pia tume nasihiwa kuwafuata na kuchukua kutoka katika mifano yao iliyomo katika Qur'aan na Sunnah mizani ya ufahamu wetu kuhusu Dini*). Hawakuwa wakiongeza chochote katika vitendo vya ibada zao za kawaida wakati wa tarehe ya kuzaliwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Lau wangeliongeza nyongeza za aina yoyote, ingelikuwa bila shaka limefikishwa kwetu. Kwa sababu walikuwa na bidii mno na wenye hamu mno kuwa na ilimu haswa ili kutenda matendo ya ibada yenye kumridhisha Allaah (تبارك وتعالى) na ndivyo walivyokuwa waliokuja baada yao; *At-Taabi'een* na *Tabi'i At-tabi'een.*

Mwanachuoni Abi Abdullah Muhammad Al-Haffar katika wanavyuoni wa ki-Maaliki alisema, "Wewe huzingatii kuwa ljumaa ndio bora ya masiku, na siku bora ya matendo ya ibada ni kufunga siku hiyo, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikataza kuifunga siku hiyo licha ya

(Endelea kwenye Uk. 2)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

ubora na thawabu ya siku hiyo. Hili laonyesha kuwa twakatazwa kubuni, kuzua kitendo cha ibada inayo ambatana na wakati au mahala na matukio yake. Kuwa wa mwisho wa ummah huu hawawezi kuwa wameongoka zaidi, bora kuliko wa mwanzo wao. Kwa yakini nasema, faida na manufaa yote nikatika kuwafuata wema wa mwanz."

KIKOMO CHA NNE: Angalia ufahamu wa hali ya juu wa Al-Farouq 'Umar Ibn al-Khatab (رضي الله عنه) kama alivyoanzisha kalenda ya Kiislamu kwa Hijra ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) Madeenah, inaonyesha kama alama ya ushindi wa Uislamu juu ya ushirikina kuliko kuanza kwa siku aliyozaliwa au siku aliyokufia. Wajuwa ni kwa nini? Ni kwa ajili ya kuipa umuhimu wa kina na hakika ya mambo juu ya ada na dasturi.

KIKOMO CHA TANO: Wa kwanza kuzua uzindiki huu katika Uislamu ilikuwa ni dola ya Faatimiyyah, Cairo katika karne ya Nne A.H – walibuni sherehe sita za mazazi (*Mawlid*); Mtume (صلى الله عليه وسلم), Ali, Faatimah, Al Hassan na Al-Husain (رضي الله عنهم) na ya sita ya Ufalme wao wakati huo kadhalika. Sherehe hizi zilibakia mpaka yalipopigwa marufuku na Al Afadal Ben Amier Al Jiyosh, kabla ya kutawala kwao tena enzi ya Al-Hakim Bin Amr Allah 524 A.H kwa wakati huo watu walikuwa wameyasahau.
Kwa hivyo taifa halikushuhudilia sherehe hizi kabla ya serikali hiyo. Suala ni kuwa, Jee! hawa Faatimiyyah wako sawa ili sisi tuwe wenye kuwaigiza na kuwafuata?
Na zaidi katika jambo la kushangaza ni kwamba kuna baadhi ya watu wenye kupendelea *Birthday* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuliko hata *Laylatul-Qadr.*

KIKOMO CHA SITA: Watu wa historia hawakuafikiana kuhusu mwezi aliozaliwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Wengine walisema ilikuwa ni Ramadhaan, lakini wengi walisema ilikuwa ni Rabi' Al-Awal, kisha wakatafautiana zaidi, kuhusu siku aliyozaliwa, na maneno mengi yakaandikwa: Ibn Abdul Bar' alisema ni tarehe mbili, Ibn Hazim alisema ni tarehe nane ambayo wengi wa Ahlul-Hadeeth wasimama nayo. Na wengine tarehe tisa iliyochukuliwa kuwa ndio yenye uwezekano mkubwa na Abu Al-Hasan Al-Nadawi na Zahid al-kawthary. Na Al-Baqeer naye alisema siku ilikuwa ni tarehe kumi ya mwezi huo. Ibn Ishaq alisema tarehe ni kumi na mbili, kuna pia kumi na saba na kumi na nane.
Tafauti zilizoko za tarehe ni ushahidi wazi yakuwa Maswahaba hawakuliona kuwa hili ni jambo muhimu ili wawape watu wa kizazi kifuatacho kuhusu siku hiyo. Na kwa ilmu yao hakuna ibada maalum ya siku hiyo. Lau kama ingelikuwa kuna mambo ya ibada haswa inayohusiana na siku hiyo, basi tungelihadithiwa kwa uswaheeh wa hali ya juu kabisa kuhusu mwaka, mwezi, siku na hata saa. Sote tunaamini yakuwa hakuna kilichopotea katika mambo ya ki-Islamu abadan.
Tukiangalia ndani ya suala hili ki-Historia, twaona yakuwa Maswahaba (رضي الله عنهم) hawakuwa wakisherehekea mazazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ya kila mwaka au sherehe za kila mwaka za Hijriyyah. Na zaidi ushahidi yakuwa hapakuwa na hizi tarehe, walitafautiana kuhusu tarehe ya kuzaliwa kwake, wakatoa tarehe mbambali. Kwa sababu walijuwa kuwa hakuna matendo ya ki-ibada fulani. Yajulikana vyema kuwa waliobora wa Ummah huu katika vizazi vya mwanzo hawakusherehekea Mawlid, bali yalizuliwa baada miaka mingi kupita. Katika ajabu ya haya ni kuwa mtawala wa Irbel alikuwa akisherehekea Mawlid ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), mwaka mmoja tarehe nane Rabi Al Wal na mwaka mwingine tarehe kumi na mbili, kwa kuwa alichukulia katika ufahamu wake tafauti zilizoko baina ya wanazuoni (Ibn Khalikan V.1 Uk.437).

KIKOMO CHA SABA: Siku aliyozaliwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na siku aliyokufa zinafanana (Rabil Al-Wal 12th Jumatatu). Kwahivyo, furaha ya siku hii sio sawa kuliko huzuni. (kama ilivyo semwa na wanazuoni wengi kama Ibn Al Haj Al Malikee na Fakhanee). Kwa mfano Ibn Al Haj Al-Malikee alisema: "Jambo la kustaajabisha mno katika sherehe zao ni kuwa, wanaweka tamasha za nyimbo na kupeana hongera ya kuzaliwa kwake, akiwa siku hiyo aliondoka kuregea kwa Mola wake peponi (Alikufa), ambayo ni siku inayosimama kama iliyo mbaya kabisa katika mahangaiko na huzuni ambayo Taifa hili La ki-Islamu limewahi kukumbwa nayo, ili na kwa vipimo wanavyotumia, wafaa kulia mno na waonyeshe mambo ya huzuni, badala ya kuimba na kuonyesha furaha na kuterema wakati huo" - (Al-Mudkhal 2/16)

KIKOMO CHA NANE: Jambo kubwa ni kuwa sherehe za Mawlid zimeenea katika mataifa ya Kiislamu yanayoambatana na mataifa ya kikristo, kama vile Egypt, mataifa ya Shaam, ambapo hao wakiristo washerehekea Christmas kama Mawlid ya Eesa na mawlid ya Ahli zake. Waislamu waliwataba (kuwaigiza) katika hayo, ambayo ndiyo iliyokuwa sababu ya kuenea kwa uzindiki miongoni mwa Waislamu. Kwa hivyo ilikuwa ni ithbati nyengine ya ahadi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) iliyomo katika hadeeth yake: *"Mtazifuata njia za wale waliokuwa kabla yenu, shubiri kwa shubiri, pima kwa pima, hata wakiingia katika shimo la kenge mtawafuata."* - tukauliza *"Ewe Mtume wa Allaah : wamaanisha Mayahudi na Manaswara? Akasema nani mwengine?* (swaheeh al-Bukhari na Muslim).

SUALA –WEWE KAMA MUISLAMU WAJIANDAA VIPI NA AHADI YA MTUME WAKO (صلى الله عليه وسلم)?
Kuwaigiza kwao kulifikia kiwango cha mwachuoni As-Sakhaawi akisema: "Pale ambapo wanaoabudu misalaba wameyachukulia mawlid ya Nabii wao (au mungu wao) kama siku kuu ya tamasha na kula na kunywa, kwahivyo Waislamu wanastahiki zaidi kuifanya siku kuu ya kunywa na kula Mawlid ya Nabii wao (صلى الله عليه وسلم) — Lakini kilio chake kilipingwa na wanazuoni wengine. Mulla Ali Al-Qarri aliisema "ushahidi yakuwa Waislamu waamrishwa kutafautiana nao sio kuwafuata na kuwaigiza... (Al-Mawred Al-Rawi 29)

KIKOMO CHA TISA: Kumpenda Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakukamiliki kwa kusherehekea Mawlid lakini kwa kuifuata Sunnah Yake pekee, na kuipa utukufu wa juu katika kila kitu. Ni lazima tuzingatie kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba wake (رضي الله عنهم) walikuwa ni bora wa *Ibaadur-Rahmaan* na walio wema mno wa Ummah huu, bila ya Mawlid walikuwa ndio bora, dini yetu yatulazimu sisi.
Hakika yakuwa sisi ni lazima tufurahike na kumridhia Mtume (صلى الله عليه وسلم) iwe ni kila siku sio siku moja kwa mwaka (ikiwa ndani ya kila siku twafuata Sunnah zake na Maagizo yake – sio

(Endelea katika Ukurasa wa 3)

mara moja kwa mwaka lakini kila siku (ikiwa mna Shirk katika kasida zao) na haraam yaliokatazwa kama nyimbo na miziki na kwenda mrama kama wafanyavyo ahlu twareka ma-Sufi, ma-Shi'ah na ma-Khurafi) twafaa kufurahi na kuyafanya na yale aliyotuagiza na kuyaacha aliyotukataza. Hilo pekee, kwa kuipa nguvu Dini yetu twapata mazuri na ufanisi wa maisha haya ya kilimwengu na kesho Akhera.

KIKOMO CHA KUMI: Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: *"Musinisifu kama wanayomsifu Manaswara Eesa Ibn Maryam, mimi ni Abdu na Rasool (mwenye kumuabudu na mtumishi wake) kwahivyo semeni Abduhu Wa Rasooluhu."*
Mengi katika yanayofanywa katika tamasha za Mawlid hupita mipaka katika kumsifu Mtume (صلى الله عليه وسلم) (kinyume na maamrisho yake). Zaidi ni ya kustaajabisha kuwa hata wanazuoni wanaowapigia debe Mawlid wakubali kuwa kuna kuvuka mipaka katika kumsifu Mtume (صلى الله عليه وسلم) nyakati za Mawlid inayokurubia *kufr* (ukafiri)!! Na haswa wakati watu wanapita mipaka yote na wakatunga vitabu ikiwa ndani mwake mna hadeeth walizozitunga miongoni mwa hadeeth *munkar* na *mawdhoo* zinazonasibiishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa mfano Abdullah Al-Ghamari, mmoja wa ma-Sufi wa enzi hizi alisema: "Vitabu kuhusu mazazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) zimejaa Hadeeth *mawdhoo* (zilizozuliwa) ambazo zimekuwa zilizo na itikadi ya nguvu katika mabongo ya watu! Nitawatajia kutunga kitabu kuhusu mawlid ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) lakini kitakuwa huru na mambo mawili: Hadeeth *mawdhoo* na maandishi ya kuchukiza ya kimashairi." Ninachokikusudia hapa nasema kuwa kuzidisha katika mambo ya ibada kwa ujumla yakatazwa katika Uislamu kama ilivyo katika aya ya Qur'aan: **"Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lililo la kweli."** [AN-NISAA 4: 171].
Nasi kadhalika tumeagiziwa hayo hayo. Zaidi, yeyote anayemsifu Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kitu kisicho na ithibati katika Dini yetu ataingia ndani ya Hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): [....*na yeyote atakaesema urongo juu yangu, basi na ajitayarishe kiti chake motoni]* – hadeeth swaheeh Al-Bukharee na Muslim)
Na ziada katika uzuri (wema na n.k), hayachukuliwi kama katika mambo ya kulegezea kamba (yaani mtu afanye atakavyo) na maana ya sifa zake au dhamira na makusudio yake yasibatwilishwe. Si mambo ya mtu kusema mimi nitatunga mambo kumuhusu Mtume nizue hadeeth. Haya ni mambo ya khatari yanayoweza kutumiwa kubatwilisha deeni ya Allaah (سبحانه وتعالى) iliyo miliki Yake na Yeye Ndiye anaye endesha. Suala hili ni la hisia kali kwahivyo Abu Mo'h Al Juwainy, aliyekuwa baba wa Al harramain Imaam alimchukulia mtu anayedanganya katika hadeeth kuwa ni kafiri na akaongeza "kwahivyo yote ya kuzidisha na mambo yanayo kila mipaka ni lazima yachomwe katika moto, ama wanao yamiliki watachomwa Jahannam!! Ewe Allah Tusamehe (haya yametolewa katika kuirudi qasidah ya Burdah ya Al Busiery). Wamo wao katika ada zao za kawaida katika kufunga tamasha zao kwa maneno ya uzindika na dua zenye kufr.

KIKOMO CHA KUMI NA MOJA:
Yanayoendelea katika Mawlidi ya ufisadi yaonekana wazi na kila mmoja, ufisadi huu ni kama: watuhumu wengine wasiounga mkono Mawlid yakuwa watu wanamchukia Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakisahau kuwa kupenda na kuheshimu mno kumeambatana na kuafikiana na Sunnah na kutupilia mbali kila uzandiki na ugeni katika dini yetu tukufu.
Pia kudansi na kutumia mbinu zilizozuliwa katika kujieleza badala ya kutumia yaliyoteremshwa!! na kutunga visa vya kutukuza sifa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika dhana na ndoto zao. (na katika haya Shaykh Ali Mahfoudh Al Azhar amesema: "Muna israfu nyingi na kupoteza mali na wakati" – Al-ibada 324.)
Na naongeza kupoteza wakati huo na pesa, kulingana na misimamo ya Kiislamu, imekatazwa na yaonekana ni dhambi kabisa. Hata katika kutenda yaliyo halalishwa kukiwa israfu huwa ni haraam- na suala ni Jee! yawaje ikiwa wakati na pesa zatumiwa katika haraam ambazo *maa anzala-LLAHU min sultwaan*??

KIKOMO CHA KUMI NA MBILI:
Kuna uafikiano baina ya Waislamu kuwa Mawlid ni uzindiki ulio-ongezwa katika Dini ya Kiislamu, lakini wanazuoni wametafautiana kuhusu hali yake, ikiwa ni jambo zuri au baya. Baadhi ya wanazuoni wamependelea kusema ni Bid'a nzuri- wakipima ati faida walizoziona!!
Ikiwa wengi wenye mielekeo ya Qur'aan na Sunnah kwa ufahamu wa walio bora wa Ummah yaani Swahaba, katika walio tangulia na wasasa kufanya Mawlidi ya Mtume ni jambo la Haraam katika Uislamu. Ni madhambi kulingana na Sharee'ah ya Kiislamu. Kwa ushahidi ambao umekataza kila bid'a katika mambo ya ibada.
Bila shaka siku kuu na siku za sherehe zazuka kutoka katika deeni wala hamna miongni mwao siku za mazazi kabisa. Hivyo basi wengi wa wanazuoni wamezuia kufungua mlango wa maovu fulani, ambayo kidogo ya watu wayaona ni hasana mazuri!! Jambo ambalo halikufanywa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala Maswahaba wala *Tabieen* wala *Atbai Tabieen* walioandamana kwa wema!! Ukitafakari kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakubaguwa baina ya Bid'a nzuri na mbaya. Alisema kila Bid'a ni upotofu.
Imaam Maalik alisema: "Kila aliyebuni uzindika ambao auona kuwa ni jambo zuri, hivyo ajifanya kuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alifanya khiana katika risala aliyotumwa nayo!! Kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) Asema: **"Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini."** [AL-MAIDAH 5: 3]
Hivyo basi ambacho hakikuwa sehemu ya Uislamu siku hiyo, hakitokuwa abadan sehemu ya Uislamu siku yoyote nyingine (kutoka Al Ia'tssam-Al Shatibi).

BAADHI YA WANAZUONI WALIOSEMA KUWA MAWLIDI NI UZINDIKI

A Imaam Al-Shaatibi katika kitabu chake (Al I'tisaam -1/3) alipotaja katika kurasa za kwanza aina fulani za uzindiki, akiyaweka Mawlid mojawapo kwahivyo akalaumu.
B Imaam Al-Fakhany
C Ibn Al Haj Al-Maliky.
D Mwanachuoni wa India, Abu Al Taib Shams Al-Haq, na Shaykh lake; Bashier Al-Deen Qannoji, aliye Andika kitabu haswa kuhusu haya. Angalia nukulu zake za Dar Qutni, juu ya hadeeth swahihi (yoyote anaye buni katika dini yetu jambo piya (ambayo asli sikatika deeni) atakanusha (ataregeshewa nwenyewe)
E Aalim Abie Abdullah Al-Haffar Al-

Maaliki kutoa Morocco alisema: “Mawlid hayakufanywa na walio bora mno baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambao ni Maswahaba zake. Hawakutofautisha baina yake na usiku mwengine wowote kwa amali yoyote. Ambayo walijifunza kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), Ambaye hakuwa akimuabudu Mola wake ila kwa yale aliyoteremshiwa –Al-Mia’yar Al-Muarab 7/99)

F Al-Allamah Muhammad Saalih Al-Uthaymeen ra alisema: “Wanafanya Mawlid kwa sababu kama wasemavyo ‘Twampenda Mtume wetu Muhammadi’. Nasi twasema ahlan wasahlan “ikiwa mwampenda” na Ahlan ikiwa mwapenda kuweka sherehe za Milaad, lakini kuwa na hadhari kuwa kuna mizani iliyoshurutishwa na Mola Wa Ulimwengu, Mbora wa mahakimu Aliyesema: **“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu. Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.”**
[Al Imraan 3: 31-32]
Kwahivyo ikiwa mtu ana Imaan na mahaba yake ya kujifanya kwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni lazima amfuate (Sunnah Yake) ama sivyo adanganya wala hampendi Mtume (صلى الله عليه وسلم), kwa sababu mizani hii ndiyo Imaan na mizani ya Hakki. Sasa wacha tutizame ikiwa Milad Nnabi yalifanywa na Mtume (صلى الله عليه وسلم)? Na Khulafaur-Rasheeeed?? Na Maswahaba wengine?? Na Atabieen?? Jibu ni Bila Shaka Laaaa! na yoyote mwengine mwenye jibu la aina nyingine twasema - Leteni ushahidi wenu ikiwa ni wakweli. Kwahivyo kwa hali hii sikufuata huko - huko ni kuzuwa - mtandao wa Ibn Uthaymeen)
Wanasema haya Mawlid yalibuniwa na dola ya Fatimi Egypt na kutoka hapo yakahamishwa sehemu nyingine za mataifa ya Kiislamu, ambapo, palikuweko na malengo ya kisiasa labada yalikuwa yamesimama mbele ya kubuni tamasha hizi. Labda kuwashughulisha Ummah na Milaad hizo na sherehe nyingine ili wasifikirie masuala ya kisiasa na masuala mengine. La twachulia Miladia kuwa matendo ya Ibada, haiwezekani ikawa hivyo kabisa!!
Hizi Miladia hamna ndani yake ila uzushi. Kumuabudu Allaah kwa kuweka hizi Miladia si Usulu katika Ibada . kwa hivyo mimi napendelea kuwa hizi sherehe zote kuwa ni uzushi. Lazima zikanushwe wala zisipewe udhuru. Kuondosha Miladia mawlid ni jukumu linalohitajika kidini na dunya. Na hiyo pia ni katika Mawlid an-Nabawee, nusu ya usiku wa Shaaban, usiku wa miiraj, laylatul Qadr na hijri mwaka mpya.masiku ya mausiku hizi zilikuwa zikichaguliwa tafauti tafauti, tamasha zikawekwa, mapesa yakamwagwa, zikafanywa hadharani kukihudhuriwa na Ummah na viongozi, na zaidi na zaidi khutbah zikatolewa, na vyakula, na mwisho husema twauhudumikia Uislamu-AJABU!!!

(Endelea kutoka Ukurasa 1)

wamefanyia utafiti kipengee hicho. Ingawa kuna mvutano mkubwa kuhusu matumizi ya sheng ama lugha simo, ni muhimu kutaja kuwa kuna baadhi ya maneno yaliyoanza kama sheng na yakaswahilishwa.
Kwa mfano nchini Kenya, Matatu ni magari ya uchukuzi wa umma ama matwana kwa Kiswahili sanifu. Vivyo hivyo, Tanzania chombo hicho kinaitwa daladala ambalo si jina la Kiswahili sanifu lakini limetiwa katika matumizi. Hata hivyo kuna hasara kubwa ya kutumia baadhi ya majina ya sheng ambayo yanapotosha maana halisi ya maneno hayo ya Kiswahili.
Kwa mfano nchini Rwanda mtu akiwa hajakamilika kwa namna moja au nyingine watu wanamuita kasorobo. Kwa hakika kasorobo ni neno la Kiswahili kumaanisha kuna upungufu wa robo ya kitu kujalizia mahali fulani kama vile dakika kumi na tano za saa na kadhalika.
Hivyo inapotumika katika mazungumzo inawakanganya waswahili. Si hayo tu, Burundi ndio kuna mambo, eti muasi kwa lugha simo ya huko ni msichana mrembo.
Kwa Kiswahili sanifu muasi ni mwanamgambo ama mtu msumbufu tu asiyeambilika wala kusemezeka.
Kenya na Tanzania ni nchi ambazo zinajulikana pia kuibuka na misimo mbalimbali na inayopotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Nchini Tanzania nilimsikia mtangazaji mmoja akisema msichana mrembo anaitwa Mkwaju. Tunavyojua katika Kiswahili mkwaju ni namna moja ya kiboko cha kumchapa mtu. Je sasa twabadilisha jina la mrembo kuwa kiboko? Mambo mawili kando kabisa. Tanzani amtu atakwambia anasikia ubao kumaanisha kuwa anaona njaa. Inavyoeleweka ni kuwa ubao ni sehemu ya mti ama mbao katika Kiswahili sanifu. Na huko Tanzania mtu anapokwambia patachimbika ana maana ya kuwa pameharibika jambo. Utata unaojitokeza hapa ni kuwa patachimbika ni kitenzi cha Kiswahili kumaanisha hali ya pengine kufanya shimo mahali ama kutoboa kitu ilhali kuharibika ni kusambatarika kwa hali ama kitu fulani. Hizo ni dhana mbili tofauti kabisa kama mbingu na ardhi.
Nchini Kenya pia mambo ya sheng yanapigiwa upatu sana hususan na vijana. Hata hivyo ni muhimu kutaja kuwa matumizi ya maneno fulani huvuruga Kiswahili Kabisa. Kwa mfano katika lugha simo Kuro ni kahaba lakini ukweli ni kuwa katika Kiswahili kuro ni mnyama wa porini wa jamii ya paa anyefanana na kulungu. Yaani hapa kosa la kwanza ni kumlinganisha binadamu na mnyama. Pili neno mbuyu Kenya lina maana ya baba lakini katika Kiswahili ni mti unaozaa mibuyu na ikiwekwa semi na iwe "kuzunguka mbuyu" basi inamaanisha kutoa hongo.
Kadhalika neno demu ambalo linatumika Tanzania, Kenya na Jamhuri ya demokrasia ya Congo lina maana ya msichana lakini katika Kiswahili sanifu ni kitambaa kinachofunika mwanamke maziwa anapolima ama tambara hivi. Je unapomwita msichana demu hujui kwa Kiswahili unamlinganisha msichana huyo natambara labda? Je huo ni uungwana? Kenya watu wanasema masa ni mama katika lugha simo lakini katika Kiswahili sanifu masa ni matendo mabaya yanayofanywa na mtu.
Athari nyingine ya lugha simo ni kuwa inaweza kuwafanya watu waache kuyatumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhania ni Sheng. Baadhi ya maneno hayo ni kama vile manzi ambalo ni neno la Kiswahili sanifu kumaanisha msichana ila wengi hulitumia kama sheng. Ashara kumaanisha idadi kumi ni sawa kwa Kiswahili lakini Kenya watu wandhania hiyo ni sheng.

MAKALA MAALUM KUTOKA KATIKA SHIRIKA LA UTANGAZAJI
BBC LONDON